

CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

(CKRC)

Verbatim Report of

**DISSEMINATION OF REPORT & DRAFT BILL, MOGOTIO
CONSTITUENCY HELD AT MOGOTIO COMMUNITY MILK DAIRY**

ON

16TH OCTOBER, 2002



DISSEMINATION OF REPORT & DRAFT BILL MOGOTIO CONSTITUENCY, HELD AT MOGOTIO
COMMUNITY MILK DAIRY ON 16TH OCTOBER 2002

Present:

Wycliffe Owade - PO Acting on behalf of Com. Dr. Adede.

Secretariat In Attendance

1. Esther Mugo - Assistant Programme Officer
2. Alice Thuo - Verbatim Recorder.
3. Paul Tukong - District Coordinator

The meeting started at 12.40 p.m.

Paul Tukong (District Coordinator): Nitamuomba Pastor Sally (inaudible) atufungulie kwa maombi.

Pastor Sally: Kwa hivyo kama uko na kofia tafadhali utoe umheshimu Mungu. Natuombe pamoja. Mungu Baba katika jina la yesu Kristo tuko mbele zako alasiri ya leo, mfalme wa Wafalme na Mungu uliyeumba mbingu na nchi. Tunakushukuru alasiri ya leo kwa sababu umetupenda hata umetujali mpaka tumekuja mbele zako alasiri ya leo. Asante Mungu wetu kwa sababu ya kila mpango ambao uko mbele yetu siku ya leo. Tunakushukuru kwa sababu wewe ni Mungu wa mipango, na hata Bwana umejua siku ya leo ya kwamba tumekusanyika mahali hapa katika Mogotio, kwa hivyo tunakushukuru kwa kila jambo ambalo liko mbele yetu. Tunasema ni asante kwa sababu jinsi vile umetujali na hata umetuongoza katika nchi yetu ya Kenya mpaka umbali huu Bwana tunasimama mbele zako. Asante hata kwa sababu ya siku ya leo, tumekusanyika mahali hapa kwa lengo na hata kwa ajili ya Katiba ya nchi ya Kenya. Kwa hivyo tunakushukuru Mungu wetu kwa sababu utatuelekeza na hata utatufanikisha tuendele kulingana na mapenzi yako. Asante kwa kila mmoja ambaye ameketi siku ya leo na asante kwa kila mmoja ambaye ako na neno la kusema siku ya leo. Kwa hivyo Mungu wetu tunaomba Roho Mtakatifu akapate kutuongoza katika hali zote na hata kwa maneno yote ambayo tunaenda kuongea siku ya leo iwe ni ya kwamba inapendekeza na hata Bwana iwe ni ya kutusaidia katika nchi yetu. Kwa hivyo Mungu wetu tunaomba ya kwamba utuongoze na utulinde katika hali zote. Naomba hayo yote nikiamini katika jina la Yesu aliye Mwokozi wetu. Amen.

Speaker: Asante, basi kwa sasa nitamualika mshirikishi ama coordinator wa tume ya kurekebisha Katiba ya Kenya katika wilaya ya Koibatek Bwana Paul Tukong ili atujulishe wageni mashuhuri na wageni kutoka hapa karibu, na wale wengine wote ambao wamewahi kufika hapa siku ya leo. Nampenda kuchukua nafasi hii, karibu Bwana Tukong.

Paul Tukong: Bwana Wycliff Awade ambaye yeye anawakilisha commissioner Dr. Adede kutoka CKRC headquarters

Nairobi na wale wote wanaandamana pamoja, DO wetu wa Mogotio, members wa constitution commission, the committee ya Mogotio, na wana constituency, the Civic Education Providers ambao wako siku ya leo, viongozi wengine wa tabaka mbali mbali wa eneo la hapa, wamama, mabibi na mabwana hamjambo? Hamjambo? Leo ni siku kubwa sana katika eneo la uwakilishi Bungeni la Mogotio kwa sababu tume ya kurekebisha Katiba kwamba wako na sisi kwa kazi ambayo bado tutaeleza nyinyi. Na kabla ya hiyo, pengine itakuwa jambo la busara na jambo la hekima, niwaonyeshe nyinyi wale ambao tunakuwa tukifanya kazi pamoja kwa mnajili ya Katiba mpya.

Basi ningeomba committee members ambao wako hapa tafadhali wasimame tupate kuwajulisha nyinyi committee members, wengine mngokuja mbele kidogo hapa, tafadhali kujeni mbele. Wanatume ambao tumekuwa tukiwasaidia nao ni kumi, wa kwanza akiwa ni mbunge wa area hii ambaye ametuma apology kama hatakua na sisi. Wa pili tuko na Bwana Charles Cheruiyot ambaye pia hayuko na sisi amesema ametuma apology. Basi na wale wako hapa tuko kwa upande ule mwingine ni Bwana Fredrick, makofi tafadhali. Bwana _____ ni commission member na anatoka area ya _____ (inaudible) anayefuata ni Councillor _____ ambaye ni chairman ya county council ya Koibatek _____ (inaudible), of course mnajua anatoka upande gani, na mama ambaye amesimama ni councilor pia Councillor Pauline Korir, huyo ni committee member na ametoka upande wa _____, makofi tafadhali. Tuko na wengine ambao hawako na sisi, bwana _____ Langat pia anatoka _____ (inaudible) amesema hatakua na sisi lakini alikuwa amesema anaweza ingia.

Ningetaka kutambua na hasa wale wengine pengine _____ ni wale ambao wamechaguliwa kuwakilisha Koibatek katika mkutano mkubwa wa Kitaifa wa Katiba ambao utafanywa kule Nairobi kuanzia tarehe 28. Walichaguliwa wiki ile nyingine kule 17 mwezi 9 kule Eldama Ravine na nipongezi kwao, tafadhali mkuje hapa mbele. Kuja hapa mbele, ni watatu walichaguliwa na hawa, hawa watawakilisha Koibatek District. Mkiona gazeti la jana la standard, majina hayo yako. Huyu ambaye ako karibu na mimi ni Bwana David Kimaiyo Kigen ni councilor wa upande wa Koibatek. Halafu hapa ni Kipingo, Charles Kipingo, anafanya kazi kule hospitalini lakini anatoka hapa hapa tu karibu na sisi, area hii ya _____ (inaudible). Wengi wamekuwa wakiniuliza Chepto Sally ni nani, ni huyo, makofi tafadhali. Yeye anatoka upande wa _____ (inaudible) akiwa yeye ni _____ makofi kwake tafadhali.

Siwezi kuwasahau wale ambao tumekuwa tukifanya kazi pamoja wakiwa waalimu wa Katiba wakizunguka eneo hili letu la Mogotio mpaka hata kule Eldama Ravine wakifanya maneno ya civic education, na wamefanya kazi mzuri sana. Wana _____ wengine wale wako hapo msimame tafadhali, naweza kuona Otoy, yes, civic division providers wale wako. Na pia Bwana Otoy Biwot, pia ametusaidia upande wa _____ (inaudible) kule _____ (inaudible). Asante.

Wageni wetu kabla hatujaendelea sana ningetaka kumualika DO wetu aje awakaribishe wageni ili tupate kuendelea na programme yetu. Bwana D.O. tafadhali. Tukaribishe bwana D.O. (*clapping*) Halafu sasa atujulishe wageni kwa sababu wageni walitangulia offisini kwake.

D.O. Moranga: Asante Bwana Tukong ambaye ni district coordinator wa Constitutional review committee. Watu wa Mogotio, yangu yatakuwa machache sana kwa sababu si baraza yangu. Nimekuja tu as a matter of courtesy ya kuonyesha kwamba sisi katika office ya Rais tunaungana na watu wa constituency kuona kwamba hii maneno inaenda vizuri hapa Mogotio.

Kwa hivyo leo sio wakati wa speeches sio wakati wa kuongea mambo mengi, ni wakati tu wa kufanya kazi ile imetuleta hapa. Hamjakuja kukaa ndio msikize hotuba ya DO, mmekuja tuu kwa mambo ya Katiba. Si ni kweli? Kwa hivyo ni kweli imepangwa, nimewaleta na ninataka niwaache na nyinyi, nimewaambia wanaweza kuongea Kiingereza, waongee Kiswahili, au kwa lugha ya mama kama wanaweza kuelewana mnaweza ongea kwa sababu kile kitu cha mhimu ni kuona kwamba mmelewana ama mmelewa ni nini wamekuja kufanya. Si ni kweli? Wakiwa ni wageni wachukuwe tu kama wageni, mkiwa na maneno wapeleke tu pole pole may be after 20 minutes mtakuwa mmelewana muongee vile wanataka na nyinyi muwaambie vile mnataka. Kwa hivyo haitakuwa ni ya upande moja itakuwa mnawaambia, mnajibu, mnawauliza, mnajibiana, kwa hivyo ni discussion. Sio mtihani, ni kitu tu mnaongea hapa.

Kwa hivyo yangu ni machache sana, ni kuonyesha ya kwamba tuko pamoja katika tutengeneze Katiba upya. Mimi nikiwa DO, office yangu ama office ya DC ama office ya PC, ama office ya Chief, Ni office moja mnataka kuongea juu yake? Ama hamjalewa tena wanasema MaDC na MaPC, na maDO na machief waende nyumbani, mmesikia hiyo? Yaani kusema mimi niende nyumba? Machief, na DC na nani, kwa hivyo, hapa hakuna kukalia mtu, unaongea siyo? Kama ni kweli mnataka hiyo office iondolewe mna? Mnasema. Saa za mchana mimi naweza wacha office nikae nisikie ni nini mlisema. Na waseme wengine saa hii wanakutana mahali pengine, kuendelea kuongea juu ya hii maneno.

Halafu wale watatu wa Koibatek wakienda Nairobi, sio kwenda kustarehe lakini kwenda kupeleka maoni yenu, yaongewe kwa urefu. Kwa hivyo hakuna hapa ati mnaweza kuogopa ati chief ako pale, hata DO alikuwa hapo, ati police, hapana, hii ni mambo ya kuongea kwa uwazi bila uoga na hakuna mtu atakuuliza ni kwa nini ulisema hii. Hapana, hiyo ni haki yako. Kwa hivyo mtu asikushitue hati kwa nini ulienda kusema hii, hapana, mimi nikiwa hapa nitakataa hiyo. Wewe sema yote, Wee sema yote yako, hiyo ni haki yako, inaitwa Constitutional right ya kusema vile ungetaka iwe. Pengine ile moja tu nitasema kwa watu wa Mogotio, ____ (inaudible) hii tutakuwa na Kenyatta day, tarehe 20th, hiyo sherehe tutafanyia hapa Mogotio, nafikiria tutafanyia hapa kwa huu uwaja, ndio hatutaenda mbali sana ndio watu waweze kuja, kwa hivyo tukutane hapa tusome hotuba ya Kenyatta Day, tuendele. Kwa hivyo mimi nataka kuintroduce wale wageni ambao wametoka head office ama office kuu ya Katiba. Tafadhali mkuje tu hapa mbele muonekane niwajulishe ndio niwaache na watu wa Mogotio mjadiliane, tafadhali.

Mseme wazee first ama wamama? Ladies first? Hata mambo ya Katiba? Sawa ladies? Equality, Sawa, hiyo ni haki yako na tutafanya vile umesema. Kwa hivyo wacha tuanzie huyu madam, yeye atusemee na nyinyi msikie vile anasema. Si ni kweli? Si ni vizuri kusikia vile anasema? Msikie sauti yake, wamama siku hizi wako na sauti. Wache tusikie sauti ya mama.

Esther Mugo: Hamjambo? Kwa majina naitwa Esther Mugo kutoka Nairobi.

Alice Thuo: Habari zenu? Kwa majina naitwa Alice Thuo kutoka Nairobi.

D.O. : Mmesikia kweli? Wanaonekana ni kama hawakusikia. Anaitwa Alice Thuo. Sawa? Hawa wanafanya kazi Nairobi na office kuu ya mambo ya Katiba, halafu tuko na ... ni mzee ama ni kijana ama ni mwanaume?

Wycliff Owade: Mwanaume. Habari zenu: Hamjambo tena. Kwa jina naitwa Wycliff Owade, nafanya pamoja na hao, na hapa nimekuja kwa niamba ya commissioner Dr. Adede. Asanteni sana.

D.O: Hiyo nikusema hivi, huyu mwanaume ndio atakuwa mkubwa kwa huu mkutano wa Mogotio. Ni kweli? Hawa wataandika maneno yote halafu wakirudi kwa office wataenda kwa computer waseme watu wa Mogotio wamesema hii, wamekubaliana na hii, wameongeza hii, au wamekataa vitu vyote ama wamekubali vitu vyote. Sawa? Kwa hivyo ako mwanaume mmoja, wamama wawili. Na ndio anakaa katikati kuona iko amani. Kipsang endelea.

Tukong: Basi makofi kwa bwana DO, hiyo ni kazi ambayo ni nzuri sana. Basi kwa wakati huu tukiwaletea kazi ambayo imetukusanyisha hapa ni kwamba leo tarehe kumi na sita tuko hapa Mogotio, hii ni programme moja kati ya zile zingine. Kuanzia week iliopita, commissioners wamekuwa nje, wamekuwa wakitembelea maeneo ya uwakilishi Bungeni kote nchini Kenya. Na leo tuko hapa, kesho tuko Eldama Ravine na programme inaisha tarehe 18 kote nchini Kenya. Asubuhi nimepatia nyinyi Constitution draft ambayo mko nayo na ninajua ya kwamba hiyo draft ambayo mko nayo, ndicho kitu ambacho tutatumia siku ya leo. Nikirudi nyuma kidogo, nataka kuwashukuru nyinyi wale wote ambao mlipeana maoni yenu wakati tume ya kurekebisha Katiba walipotembelea eneo la uwakilishi Bungeni Mogotio. Nakumbuka sana ilikuwa mwezi wa saba tarehe tano, basi kuanzia hapo, commissioners walienda kule Mombasa, wakaenda wakaweka pamoja maoni yenu yote na wakaweka katika draft ambayo tayari imetolewa. Kazi ambayo iko basi, kazi ya leo basi ni kuangalia hiyo draft, na hiyo it shall be taken through ama tutapelekwa kuangalia hiyo na Bwana Awade. Kwa sababu najua saa imeenda sana nataka kukaribisha bwana Awade ili tupate kuanza kazi yetu. Asante.

Wycliff Awade: Basi hamjambo tena wananchi? Nitaanzia kushukuru nyinyi wote ambao mmepata nafasi ili mkuje hapa siku ya leo ili tujadiliane kuhusu mambo haya ya Katiba. Katiba ni jambo umhimu sana katika maisha ya binadamu na vile coordinator amenena, mwezi wa saba mlitoa maoni, sisi tukakaa huko Nairobi natukachukua hayo maoni pande zote za nchi hii ya Kenya halafu tukaandika report, kutoka kwa hiyo report tuko na hiyo draft bill ama mswada wa Katiba. Na ninadhani nyinyi nyote mko na hizo copies. Na ningependa tuende hivi, tuko na twenty chapters hapo na tutaanza kuanzia chapter one mpaka mwisho. Kwa hivyo nimeomba mnisamehe na mniruhusu nikae chini saa ile tunajadiliana. Mmekubali? Asanteni sana.

Ya pili ni kuomba msamaha tumechelewa, tulikuwa na shida ya gari huko Kureisoi, lakini tumefika. Sasa asanteni sana, naomba mtulie ili tujadiliane na msikie sawa sawa yale maneno yako ili tusiwe na mambo kusema chini chini, mambo kama DO amesema lazima isemwe watu wote wakati wa mchana. Si ndivyo? Haya, Asante, Sasa naomba nikae chini halafu tuanze.

Okay sasa, tuangalie page 2 kwa hiyo pull out – hiyo gazetti mko nayo, uangalie hiyo page 2, nitaongea na Kizungu na Kiswahili kidogo kidogo. Tuko pamoja? Page 2 imeandikwa hapo,

Preamble. Preamble, yaani foundation ama mwelekeo wa hii Katiba yetu, tujue Katiba ni nini ama nini iko ndani ya Katiba. Hii Katiba inahusiana na mambo kama gani? Sasa huu ndio mwanzo mwanzo ya hii Katiba na nitasema hivi kwa kiswahili- Preamble – yaani utangulizi, na inasema hivi: Sisi wananchi wa Kenya tukifahamu wingi wa sauti zetu za kikabila, utamaduni na kidini na tukidhamiria kuishi kwa amani na umoja kama taifa moja huru lisilo gawika, tukijitolea kulea na kulida masilahi ya kila mmoja, familia na jamii katika taifa letu tukitambua matumaini ya wanawake na wanaume wetu, ya kuwa na Serikali ambayo imejengwa katika misingi muhimu inayodhamini uhuru, democrasia, haki ya kijamii, na utawala wa sheria; tukitekeleza haki yetu isiotendeka ya uhuru ili kuamua aina ya utawala wa nchi yetu na tukiwa tumeshiriki kikamilifu katika utaratibu wa kuandaa Katiba. Tunaikumbali, tunaifanya sheria, na tunaitoa kwetu wenyewe na kwa vizazi vyetu vijavyo Katiba hii. Mungu ibariki Kenya. Sasa huo ndio mwanzo wa hii Katiba yetu. Tuko pamoja?

I want now to take you to page 4 chapter one na imeandikwa hapo: Sovereignty of the people and supremacy of the Constitution. Nataka kujua nini mamlaka ya Katiba, inatoka kwa watu gani? Na imeandikwa hapo, Sovereignty of the people and supremacy of the Constitution. Nitasoma kwa kiswahili, bado article one one. Mamlaka yote ya uhuru ni ya wananchi wa Kenya na yanaweza kutekelezwa tu kulingana na Katiba. Tuko pamoja? Mamlaka haya ya Katiba ni ya wananchi wa Kenya, ni nyinyi wenyewe Wanakenya. Sasa nyinyi wananchi tumepatia viongozi katika sehemu mamlaka.

Halafu tusome hapo NO. 3, article one No. 3. Mamlaka ya uhuru wa wananchi yamegawanywa kwa njia tofauti miongoni mwa kwanza (a) Bunge, ambamo wananchi wameweka imani ya mamlaka ya kisheria ya jamhuri ili yatekelezwe kwa mujibu wa sura ya saba. (b) Mamlaka ya nchi ambamo wananchi wameweka amana ya mamlaka ya kutawala ya jamhuri ili yatekelezwe kwa mujibu ya sura ya nane. (c) Mahakama – Mahakama na mahakama zingine ____ (inaudible) pendelea ambazo kwazo wananchi wamepewa amana ya mamlaka ya kimahakama ili yatekelezwe kwa mujibu ya sura ya sita. (d) Tume za kikatiba na afisi ambazo zimeundwa na sura ya kumi na saba, na kwingineko katika Katiba ambazo kwazo wananchi wamepewa amani ya kulinda na kujenga jamhuri ya kikatiba ambayo inaweza kupatikana kutokana na utekelezaji wa vyombo vilivyo vyenye majukumu na uwezo vilivyowekwa na Katiba.

Halafu ile ya mwisho ni ile inasema, haki ya kutekeleza uhuru haitatolewa kwa mtu yeyote, vikundi, wala tabaka, na hakuna mtu atakaye jitwika yeye mwenyewe au atakaye tkeleza mamlaka yoyote ya nchi ambayo hayatokani na Katiba. Na saa hiyo ndio sovereignty of the people and supremacy of the Constitution na tuna two codes. Sasa tumejua ya kwamba mamlaka yote inatoka kwa nyinyi wananchi wa Kenya. Tuko pamoja? Alright.

Now we go to chapter 2 which is about the republic. We want to know what the republic is all about. Katiba inasema nini kuhusu republic ama jamhuri. Inasema hivi: Article 6 (1) Inasema hivi: Kenya ni jamhuri iliyo uhuru. (2) Jamhuri ya Kenya

imejengwa katika msingi ya kijamhuri ya utawala mwema kupitia demokrasia ya vyama vingi, utawala shirikishi, uwazi na uajibikaji, utengenezaji wa madaraka, haki za binadamu, uhuru wa kimsingi na utawala wa sheria. Sasa hiyo ndio inaongea juu ya jamhuri. Sisi tungependa kusema, hii Kenya ni ya watu wote, na ni Wakenya wote. Hiyo ni ukweli ama urongo? Kenya ni watu wote na hata tukipata hata saa hii, tukienda kwa uchaguzi mpya, hata kwa Serikali mpya, Katiba inasema hivi, Kenya ni wananchi wote wa Kenya. Kila upande wa Kenya, Kenya ni ya watu wote wa Kenya, na Jamhuri na ni jamhuri iliyo uhuru. Kwa hivyo nyinyi wananchi ndio mko na hiyo mamlaka ya Katiba na ndio mumepatia hiyo Katiba mamlaka. Tuko pamoja?

Sasa nataka twende chapter 3 which is National goals, values and principles. But just before that, perhaps I could say something about the National Bill, and as the DO told you and the District Coordinator, this is just a draft, huu ni mswada tu, hii si Katiba, ni mswada tu. Tuko pamoja? Kwa hivyo tutasoma hii, the purpose yetu hapa, kama mtu anafikiria hiyo si sawa sawa, una haki ya kusema. Tumeelewana hapo vizuri?

Sasa tuangalie hiyo page 4 article 13, imeandikwa national days. Na nitasoma hivi, that is article 13 – siku za taifa: Siku zifuatavyo zitazingatiwa kama sikukuu ya taifa, (a) June 1, sikukuu ya madaraka, (b) December 12 – sikukuu ya jamhuri, (c) Siku ya Katiba kufanywa kuwa sheria – itaitwa sikukuu ya Katiba. – hivyo ni siku tatu lakini tuko na siku zile tunaita kama public holidays, hizo zitabaki. Sasa hapo mtasikia vizuri mkiwa na swali ama any comments, mtaleta baadaye. Hiyo chapter 3 national goals, values and principles, tuko pamoja?

Malengo ya taifa, maadili na kanuni, tunataka kujua hii Katiba inasema nini katika hayo malengo ya taifa, maadili na kanuni kwa viongozi na wananchi wa Kenya, na nitasoma kwa Kiswahili. Malengo ya taifa, maadili na kanuni, article 14 (1) Malengo ya taifa, maadiri na kanuni zilizomo katika sura hii zinahusu mamlaka ya nchi, Bunge, mahakama, utawala wa wilayani na vyombo vingine vya Serikali na viongozi. Raia na miungano wa kibinafsi pale ambapo vyombo imojawapo ni hivyo. Hivyo mnaweza kusoma lakini lengo kubwa hapa ni ku-understand kwamba kiongozi yeyote na kwa kila raia yeyote razima kuwa kuna malengo, maadili na kanuni. Tuko pamoja? Hapo mnaweza kusoma.

Sasa twende kwa article 16 that is page 5 – duties of a citizen. Not chapter 15, article 15 (25) Kwa kiswahili, wajibu wa raia, in other words, inasema hivi: hata ingawa kuna Katiba, hata ingawa tutaongea kuhusu maneno ya Rais, ya wananchi wa Kenya, ni wajibu wenu nyinyi Wakenya mjue ya kwamba mko na role ya kuplay, mko na wajibu kama raia kuwasaidia nchi hii ya Kenya.

Si tu kwamba sasa Katiba iko, lakini bado naangalia tu vile mambo inaendelea. Tuko pamoja? Mko na wajibu kama wananchi wa Kenya na sheria inasema hivi: Article 15 (1) Ili kutimiza malengo ya kitaifa, maadili na kanuni, raia wote wana wajibu wa (a) kujifahamisha kuhusu masharti ya Katiba na kudumisha maadili na malengo yake. (b) Kutetea na kuulinda Katiba na sheria. (c) Kutekeleza haki yao ya kidemokrasia kwa kupiga kura na kushiriki katika namna zingine kwa shughuli za kisiasa – kwa kupiga kura, hiyo ni maneno mhimu sana. (d) Kushiriki Katika kazi ukiwemo ujenzi wa familia ili kujikimu na kulinda masilahi

yao na familia zao kwa manufaa ya jumla na kuchangia katika maendeleo ya taifa. (e) Kukuza uwezo wao kadri wanavyoweza kupitia (inaudible) maarifa, kuendelea na masomo na utunzaji wa usitadi. (f) Kuchangia masilahi na maendeleo ya jamii wanapoishi (g) Kujitahidi kukuza umoja wa kitaifa na kuishi kwa amani na wengine. (h) Kuendeleza udemokrasia na utawala wa sheria au (i) kuendeleza maisha ya kifamilia na kusema kwa heshima katika mikitaba ya familia. (j) Kulinda na kutunza mali ya uma ili isiharibiwe wala kutumiwa vibaya. (k) Kulinda mazingira na kuhifadhi mali ya asili. (m) Kushirikiana na vyombo vyo kutekeleza sheria ili kudumisha amani na sheria. (n) Kujiepusha na vitendo vya ufisadi (n) Kuelewa na kukuza nafasi ya Kenya katika jamii ya kitaifa. Kwa hivyo majikumu yaliyoelimishwa katika kifungu moja, yanayohusu pia pale inapobidi wale wasio kuwa raia. Sasa hiyo ni wajibu wa raia. Tuko pamoja?

Twenda kwa uraia, yaani citizenship that is chapter 4 – uraia. Tunataka kujua, hii maneno ya uraia, Katiba mpya inasema nini? Na nitasoma kwa Kiswahili kwa kifupi tu. Article 15 (1) inasema hivi, kanuni za kijumla kuhusu uraia – isipokuwa pale ambapo Katiba inaweka mashariti tofauti, raia wote wa Kenya (a) Wana haki sawa ya kupata haki, (inaudible) na faida za uraia. (b) Wana kiwango sawa cha wajibu na majukumu ya uraia na (c) wana haki sawa ya kupata passport ya Kenya na kupata haki yeyote ile ya kitaburisho inayotolewa na Serikali kwa uraia. Halafu tunataka kuona zile classifications or acquisitions of citizenship na tuko na three categories. Kupata uraia – hapo article 18 – uraia unaweza kupatikana kwa njia ya (a) kuzaliwa – yaani uraia wa Kenya. (b) Kusajilishwa na (c) kuandikishwa. Halafu inasema nini? Article 19 (1) uraia kwa kuzaliwa – citizenship by birth. Kila mtu aliyezaliwa baada ya utekelezaji wa Katiba atakuwa raia wa Kenya ikiwa wakati wa tarehe ya kuzaliwa mtu huyo mama ama baba yake ni raia wa Kenya. Tuko pamoja? (2) Mtu aliye raia wa Kenya kuambatana na (inaudible) hii hawezi kupokonywa uraia wake – yaani tuko na citizenship by marriage – uraia na ndoa. Article 21 – Katiba mpya inasema hivi: Mtu aliyefunga ndoa na raia wa Kenya kwa kipindi kisichopungua miaka mitatu ana haki ya kusajilishwa kama raia wa Kenya akituma ombi. Pili uraia haupotei kwa njia ya ndoa ama wakati wa talaka. Hizo ni recommendations zenu.

Halafu kuna ule uraia kwa kuandikishwa, article 21 – mtu aliyekuwa mkazi wa Kenya kisheria kwa mfululizo kwa kipindi kisichopungua miaka saba na ambaye anatosheleza masharti yaliyotolewa na sheria ya Bunge, anaweza kutuma ombi la kuwa raia wa Kenya kwa kuandikishwa. Tuko pamoja?

Halafu tuna ile sheria ya uraia, kuhusu watoto wanaopatikana Kenya na watoto wa kupanga. Tuko pamoja? Article 22 (1) inasema hivi:- mtoto anayepatikana Kenya ambaye yuko chini ya umri wa miaka minane ambaye wazazi wake hawajulikani atachukuliwa kuwa raia wa Kenya akiwa chini ya umri wa miaka minane. Pili mtoto aliye na umri wa chini ya miaka kumi na nane ambaye anaishi na raia wa Kenya ana haki ya kuwa raia wa Kenya anapotuma ombi.

Uraia mara dufu, yaani dual citizenship – wakati tulipotembelea katika constituencies zote za nchi ya Kenya tulipata kama wale ndugu zetu Turkana, Somali, Rendile, na kila mahali na walikuwa na maoni tofauti tofauti kuhusu uraia mara dufu. Na ninataka nisome hivi: Article 23 (1) inasema uraia mara dufu unaruhusiwa chini ya sheria ya Kenya. (2) Mtu anayepoteza uraia wa

Kenya kwa ajili ya kupata uraia wa nchi nyingine, wa kabla ya kutekelezwa kwa Katiba hii ana haki ya kufajiliwa kama raia wa Kenya anapotuma ombi lake. (3) Mtu anayepoteza uraia wa Kenya kwa ajili ya kupata uraia wa nchi nyingine anapowacha uraia wa ile nyingine atakuwa na haki ya kurudia uraia wake wa Kenya ambao aliyo uraia mwanzoni. Hiyo tumeelewana vizuri?

Halafu twende kwa article 24 – Kuachishwa uraia – mtu atapokonywa uraia wa Kenya ikiwa tu ameupata uraia huu kwa udanganyifu, (inaudible) uwango, kuficha kwa hoja mhimu, ama kwa njia nyinginezo kinyume cha sheria. Sasa hiyo pia inahusu hiyo. Hizo zingine mnaweza kusoma.

I want now to take you to chapter 5 – the bill of rights - That is page 6 – the bill of rights, yaani sheria ya haki. Halafu ningependa kusema hivi, ni muhimu kwa nyinyi wananchi wa Kenya hasa kama saa hii ambayo tunaingia kwa uchaguzi na kwa hiyo Serikali mpya, mjue kwamba ni haki zetu, sisi raia ni muhimu tujue haki zetu ni nini katika Katiba. Tuko pamoja? Sasa sheria inasema nini? The bill of rights? Sheria ya haki. Na nitasoma kwa kiswahili. That is article 29 (1) Sheria ya haki ndio nguzo ya mzingi ya Serikali ya kidemokrasia na ni muundo wa ukubalifu wa maswala ya kijamii, kiuchumi na kitamaduni. (2) Madhumuni ya kutambua na kulinda haki za binadamu ni kuhifadhi hati ya utu, ya watu binafsi, ya jamii, na (inaudible) vipawa vya binadamu wote.

Sasa haki na uhuru ule ulitolewa katika sheria za haki ni hizi. (a) ni wa kila mtu na hautolewi na Serikali. (b) Hauwachwi nje, haki nyinginezo ambazo hazikutajwa moja kwa moja katika sura hii na (c) unahusika tu katika (inaudible) ulitolewa katika sheria hii. Na ningependa tena kuongeza kwamba itakuwa Katiba inasema kwamba Serikali lazima ilinde hiyo haki ya wananchi kwa njia zozote. Tuko pamoja?

Sasa hizi zingine mtasoma lakini ningetaka kupeleka nyinyi kwa vikundi vingine ambayo hii Katiba imetaja. Na taka kwanza nianze na article 32 the same page 15 haki ya kuishi – nataka kujua sheria ya sasa inasema nini – haki ya kuishi 32 (1) Kila mtu ana haki ya kuishi kwa nchi hii ya Kenya (2) Hukumu ya kifo imefutuliwa mbali – hilo ni pendekezo letu – hukumu ya kifo imefutuliwa mbali. Article 33 inasema – Kila mtu yuko sawa mbele ya sheria na ana haki sawa ya kulindwa na usawa wa mafanikio ya sheria. (2) Usawa unajumulisha kufurahia kikamilifu usawa na wa haki zote na uhuru wote. Uhuru kutokana na ubaguzi – baado iko article 34 – Serikali haitabagua kwa maonefu ya moja kwa moja ama kwa njia isio kuwa dhahiri kwa mtu yeyote kwa sababu moja au zaidi pamoja na jamii, jinsi, muja mzito, ndoa, kabila, ama hali ya kitabaka. rangi, umri, ulemavu, dini, dhamira, imani, utamaduni, lugha ama kuzaliwa. Tuko pamoja?

Haya twende kwa akina mama ama wanawake – article 35 – Nakumbuka hii ilikuwa ni maoni ya wananchi wa Kenya na tumejaribu kusamarize hapa. Sasa Katiba mpya inasema hivi kuhusu wanawake article 35 (10) Wanawake wana haki ya kutendewa sawa na wanaume, pamoja na haki ya kupata fursa sawa katika siasa, uchumi, na shughuli za kijamii. (2) Wanawake wana haki ya kupewa hadhi ya utu sawa kama ile inayopewa wanaume. (3) Wanawake na wanaume wana haki

sawa za kurithi, kupata nafasi ya kupata na kudhibiti mali. (4) Sheria, utamaduni, desturi ama mila zozote zinazorotesha hadhi ya utu, ustawi na maslahi ama hali ya wanawake zimepigwa marufuku. (5) Serikali italeta wanawake na haki zao, kwa zingatia hali zao maalum na jukumu lao la kuwa mama katika jamii. No. (d) itapewa vifaa vinavyotosheleza na fursa ya kwendeleza masilahi ya wanawake ili kuwawezesha kufikia upeo wa vipawa vyao na maendeleo.

Halafu tuna wazee katika jamii, katiba mpya inasema hata hawa wazee wana heshima, wana akili, na hiyo akili yao lazima tu-respect, na lazima pia Serikali ilinde maisha ya wazee. Na inasema hivi article 36 (1) Wazee katika jamii wana haki ya kwendelea kufurahia haki zote na uhuru kama ilivyofafanuliwa katika sheria ya haki pamoja na haki ya (a) kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii. (b) Kufuatilia maendeleo yao kibinafsi. (c) Kuwa uhuru kutokana na aina zote za ubaguzi, unyanyasaji dhuluma ___ (d) Kuishi kwa heshima na utu na (e) Kubaki na uhuru wao. Zingine mnaweza kusoma lakini kitu mhimu ni kwamba Serikali lazima ilinde wazee kwa maisha yao yote. Hiyo sasa Katiba mpya imeweka.

Article 37 (1) Watoto wana nafasi maalum katika jamii – ni jukumu la wazazi wao, na nitarudia ni jukumu la wazazi wao, ukoo, jamii na Serikali kuwalea, kuwalinda na kuwaelemisha ili waweze kuendelea katika mazingira salama na katika hali ya furaha, upendo, heshima, na maelewano na waweze kutimiza upeo wa vipawa vyao katika hali zote, kimwili, kiakili, na kiroho kwa manufaa yao wenyewe na jamii kwa jumla. Kwa hivyo hata hii ni Katiba mpya, inalinda watoto na mwende nyinyi nyote msome hizo, because Katiba mpya inapendekeza nini kuhusu watoto.

Tuende kwa familia article 38 (1) page 7 familia – nitasoma kwa kifupi – article 38 (1) Serikali itambue familia kuwa ndio msingi wa umoja wa kijamii na ndio msingi muhimu wa taratibu za kijamii. (2) Familia inasitahili heshima na ulinzi wa Serikali. (3) Kila mtu mwenye angalao umri wa miaka 18 nitarudia, Kila mtu mwenye anga lao umri wa miaka 18 (a) ana haki ya kuoana au kuolewa kulingana na makubaliano. *End of side A*

Ama wana haki sawa katika ndoa wakati wa kuoana kwao na katika kuvunja ndoa yao. Tuko pamoja?

Basi twende kwa walemavu article 39 – walemavu, Katiba mpya inalinda pia walemavu na inasema hivi kwa kifupi – walemavu wana haki ya kufurahia haki zote na uhuru wote uliotajwa katika mswada huu wa sheria na kushiriki kikamilifu katika jamii kama wengine. Na hata mtaweza kusoma hiyo mjue sheria inasema nini kuhusu walemavu.

Nataka kwenda kwa article 44 (1) the same page 7 article 44 (1) Uhuru wa dini, imani na maoni, sheria inasema nini? Katiba inasema hivi: article 44 (1) Kila mtu ana haki ya uhuru wa dhamira, mawazo, imani na maoni. Hapo pia unaweza kusoma ujue inasema nini. Haya twende kwa page 8 tuko na page 8 article 45 – freedom of expression and above there we have publication of opinion and down there we have access to information, and then up there we have freedom of association. Are we together? We have freedom of expression, publication of opinion, access to information, and freedom of association. What it simply says, is that we as the people of Kenya should have access to any information, Are we together? We the people

of Kenya should have access to any information, be it newspapers, be it bulletins in the radio, be it channels to the television.

Hakuna mtu ama hakuna vyombo vyoyote vile vya habari ambavyo vitajificha kitu, kila kitu kiwe kibaya ama kizuri, kitakuwa wazi. Tuko pamoja? Halafu wannachi ndio wataamua tuingie ama tufuate njia gani. Na mna haki kufuata hiyo. Tuko pamoja?

Sasa Katiba inasema kila mtu ana uhuru kupita tuseme kuuliza kwa habari yeyote ama kuuliza maneno yeyote ambayo iko na shida kwa kila chombo katika nchi yetu ya Kenya. Tena kwa bill of association inasema ya kwamba kila Mkenya ana haki kujiunga na association yeyote, ikiwa ni chama cha kisiasa, ikiwa ni any welfare group, ama association ingine, mna uhuru kuingia kwa hiyo na hilo uhuru lazima ilindwa na Katiba. Tuko pamoja? Kwa hivyo sasa hiyo ndio maana ya freedom of association, freedom of expression, na publication of opinion.

I want now to take you to page 9, page 9 is talking of other freedoms which the state is required by law to give to the people of Kenya and I will just want to read them, other details you will get on your own. Nitasoma kwa Kiswahili, inasema hivi, kwanza article (56) tuko na social security, yaani usalama wa kijamii, tuko pamoja? Serikali lazima iangalie hiyo na ilinde usalama wa kijamii. Halafu tuko kwa article 67 on health, afya, inasema hivi: kila mtu ana haki ya afya inayojumuisha haki ya huduma za afya ikiwa ni pamoja na utowaji wa huduma za afya za uzazi. Tuko pamoja? Hakuna mtu atakayenyimwa matibabu ya dharura.

Halafu twende kwa elimu, education inasema hivi: kila mtu ana haki ya kupata elimu ya kimsingi inayojumuisha elimu ya kabla ya msingi, elimu ya mzingi na ya upili. Halafu tuende kwa nyumba – housing, 59 (1) inasema hivi – kila mtu ana haki ya kuwa na nyumba ya kukaa article 60 – chakula: - inasema hivi, kila mtu ana haki ya kutokumbwa na jaa na kuweza kupata chakula cha kutosha na bora na kukubaliwa kitamaduni. Tuko pamoja?

Halafu maji, 61 – kila mtu ana haki ya kupata maji ya kutosha na bora.

No. 62 – Usafi, kila mtu ana haki ya usafi inayotosheleza ikiwa ni pamoja na uwezo wa kuwazika watu kwa njia ya heshima.

Article 63 – Mazingira: - kila mtu ana haki ya mazingira yaliyo salama kwa maisha na afya. Zingine tutasoma tukienda kwa ile chapter ya mazingira. Kwa hivyo hivyo ndio umuhimu tusome kabla hatujamaliza hiyo bill of rights nataka tusome hiyo article 64 (1)

Article 64 (1) Haki za wateja yaani consumer rights – ni vizuri nyinyi wananchi wa Kenya mjue rights zenu kama wateja na inasema hivi – Wateja wana haki ya (a) kupata vifaa na huduma zinazofaa. (b) Kupata habari inayowafaa ili waweza kunufaika kikamilifu kutokana na bidhaa na huduma. (c) Kulindwa afya yao, usalama, na masilahi yao ya kiuchumi. (d) Kulipwa fidia kwa makosa yanayosababisha hasara au majeraha. (2) Wanaotoa huduma watajitahidi kutafuta ushauri kutoka kwa wateja na vyama vya wateja kuhusiana na maswala yanaouwathiri. Tuko pamoja? Sasa hizo ndizo za wateja, ili nyinyi kama wananchi

wa Kenya mjue haki zenu kama wateja mlindwe.

I want now to take you to page 10 article 70 – rights of persons held in custody. Yes, the coordinator is reminding me mtakuwa na saa ile ya kuuliza maswali, sasa saa ile tunaongea ili tuende haraka haraka, mna mark tu pahali mko na maneno. Hiyo ni sawa? Ili tuende haraka haraka badala ya kuuliza maswali saa hizi. Tuko pamoja? Very good.

Sasa tuende kwa article 71 – rights of persons held in custody. Clause (1) Haki za watu walio kizuizini. Inasema hivi, watu wote walio kizuizini chini ya sheria wawe wamehukumiwa au la wataendelea kuwa na haki zao chini ya Katiba isipokuwa haki hiyo iwe haimbatani na uhalisi wa kuwa kizuizini. Tuko pamoja? Sasa hizo zingine mnaweza kusoma baadaye.

I want now to take you to chapter 6: representation of the the people, I will just read to highlight you on your right as a Kenyan so that you are aware of what the new Constitution is saying about the bill of rights. Therefore it will only be logical to follow it with the representation of people which is on page 11. Sitasoma zote but I will just highlight the main issues ili mjue hasa wakati huu wa uchaguzi, mjue juhudi zenu, ama wajibu wenu kama raia wa Kenya ni nini. Na tusome hiyo the rights to vote – article 78 (1) Just down there, inasema hivi – Haki ya kupiga kura, article 78 (1) Raia mwenye umri wa miaka 18 na zaidi ana haki ya kupiga kura. Tuko pamoja? That is you go to page 20 then we have qualifications for registration as a voter: that is article 79 (1) Raia anastahili kusajiliwa kama mpiga kura kwa uchaguzi, kama kufikia siku ya maombi ya usajili raia huyo. (a) Ana umri wa miaka 18 na zaidi. (b) Kuwa kawaida amekuwa mkazi katika jamhuri (c) Kwa muda usiopungua mwaka mmoja kabla ya siku hiyo (2) Kuwa jumla ya kipindi kisichokuwa chini ya miaka nne katika jumla ya miaka minane kabla ya siku hiyo. (c) Kwa muda wa vipindi vinavyolingana na muda usiopungua miezi mitano kwa mwaka kabla ya siku hiyo. (d) Kwa kawaida amekuwa mkazi kwenye eneo Bunge ambapo ombi la usajili lilipofanywa au (e) Ameajiriwa kazi, anaendesha biashara au ameminiki ardhi kihalali au nyumba ya kukaa kwenye eneo Bunge hilo. Tuko pamoja?

I want to take you to article 81 – na ni mhimu sana msikilize hiyo, article 81 Katiba mpya inasema nini? Inasema hivi – katika kila uchaguzi, tume ya uchaguzi itahakikisha kuwa (a) utaratibu wa uchaguzi ni mwepesi na rahisi. Tuko pamoja? (b) Sanduku la kura nangavu (c) Kura zinahesabiwa, zinaorodheshwa na kutangazwa na msimamishi kwenye kituo cha kupiga kura. Tuko pamoja? Kitatangazwa hapo hapo siku ya mchana huyo. Tuko pamoja? Wazi wazi, hakuna hii maneno ya kupeleka mahali, hapo hapo tu, tuko pamoja? Basi sasa hii ndio inaongea juu ya uchaguzi ama kuwa voter..

Halafu tuna hiyo tume ya uchaguzi ambayo tutasoma baadaye lakini ningependa kusema hivi, majukumu ya tume ya uchaguzi that is article 84 (1) tujue sasa kwa Katiba mpya, majukumu ya tume ya uchaguzi zitakuwa ni nini. Tume ya uchaguzi ina wajibu wa (a) Usajili wa kuendelea wa wapiga kura. (b) Kuweka mipaka ya maeneo Bunge (c) uwendeaji usimamizi kwa uchaguzi na kura za maoni. (d) Uendelezaji wa uchaguzi na kura za maoni, uhuru na zenye usawa, (e) Usimamizi wa niaba ya kisiasa. (f) Usimamizi wa mfuko wa fedha za kisiasa. (g) Usuhulisaji wa ubishi wa uchaguzi (h) Uendelezaji wa elimu ya raia, na utamaduni wa demokrasia na (i) Kusaidia katika uchunguzi, ufuatilizaji na (inaudible) wa uchaguzi.

Halafu hapo tuna vyama vya kisiasa, that is article 87 – mnaweza kusoma lakini nitasoma

Kwa ufupi haki ya kuunda chama cha kisiasa. That is on page 12 article 87 – Kwa mujibu wa (inaudible) hamsini raia yeyote ana haki ya kuunda chama cha kisiasa. Pili chama cha kisiasa kina haki ya msaada wa kifedha kutoka kwa Serikali kuwa mzingi ulioangizwa na sheria ya Bunge. Tuko pamoja? (3) Hakuna mtu atakayetumia rasli mali za taifa kusaidia chama cha kisiasa. (4) Bunge litahidhinisha sheria inayoangiza masharti kwa vyama vya kisiasa. Yaani kwa hii Katiba mpya tuna zile streamlining ama tuna zile kanuni ama sera ambazo zitalinda hivi vyama vya kisiasa. Si tu kwamba kuna wengine ambao wana chama cha kisiasa lakini ni ya ile tunaita briefcase, ile mfuko tu, but ni personal tu na wanafanya vile wanavyotaka, na hata ukitaka kujua maneno ya pesa ilitumika namna gani huwezi kujua na wewe ndiye mwanachama wa chama hiki. Hiyo ni kweli ama apana? Sasa mnasema mambo mengi imeenda vibaya sana katika chama cha kisiasa na lazima tuweke discipline ili chama ya kisiasa kifanye kazi sawa sawa na hizi zitakuwa kwa vyama vyote vya kisiasa. Tume ya uchaguzi itakuwa na jukumu kulinda hivi vyama vya kisiasa kwa vile wanaendesha shughuli zao. Tuko pamoja?

Iwe ni mfuko wa vyama vya kisiasa, fedha zingine za vyama vya kisiasa, iwe ni masumuni ya mfuko, iwe ni huduma mingi ya vyama vya kisiasa, iwe nidamu ya chama, hizo zote tume ya uchaguzi itaangalia. And I want you to look at article 98 tujue inasema nini, page 13, article 98 nidhamu ya chama, tuone inasema nini katika Katiba hii.

98 (1) Katiba au idara za ushirikiano za chama cha kisiasa zitakuwa na masharti yatakayohakikisha kuweco kuwa nidhamu chamani na yanayoambatana na kanuni za kidemokrasia, haki, na uongozi wa Kisheria, ili chama cha kisiasa hakitamuaadhibu mBunge wa chama kwa sababu ya jambo alilosema Bungeni katika utumiaji wa fadhila za uhuru wa kutoa maoni Bungeni. (3) Chama cha kisiasa kitatekeleza shughuli zake kwa njia inayoendeleza demokrasia na njia za amani. Kwa hivyo hiyo ni kuhusu chama cha kisiasa.

I want now to take you to chapter 7 which is Parliament yaani Bunge. Mjue Katiba mpya inasema nini kuhusu Bunge. Sasa nitaongea kwa kizungu kidogo halafu ni require marafiki wangu kunisaidia kuiteprete kwa kiswahili. Hiyo ni sawa?

Now, when we were crossing the constituencies within the republic of Kenya, we have got 210 constituencies in Kenya. Kenyans kept on giving us their views on how they want the structure of the new Parliament to look like. So people gave us various views and out of those various views we came up with the following: In the new Constitution, we are recommending the following: that Parliament be made of two houses. Are we together? Parliament be made of two houses:- the first house which is known as the upper house will be known as the National Council – baraza la kimataifa.

(2) The lower house will be known as National Assembly yaani ile kama ile Bunge ya kisasa.

Now what is the composition of the National Council? The composition of the National Council is as follows: National

Council will be composed of 100 Members of Parliament. Are we together. It will be composed of a 100 Members of Parliament. How will this one be done? We have got 68 districts in this country of Kenya, now 68 districts it means each district will have a representative to the National Council. If we have 68 districts it means we shall have 68 Members of Parliament. Are we together? Now, the other two to make it 70 will be representatives from Nairobi; in other words Nairobi is classified as a district just like any other district in Kenya. Are we together? So that will make the total to how many? 70. How many are remaining? 30, so what we are saying, we have 70 districts in Kenya including Nairobi we are saying of the 70, 68 will have 68 representatives and the other two will represent Nairobi. Right?

The other 30, the new Constitution recommends *tupatie akina mama*. Are we together? So *akina mama watakuwa na 30* people katika hilo Bunge la kimataifa, yaani National Council. Are we together on the National Council? If you have any problem or clarification you can raise later. Let us now go to the lower house, ama ile Bunge ya kawaida ya 210, tunasema hivi:- The current structure of the current Parliament will remain. We shall have 210 Members of Parliament as they are now representing various 210 constituencies in the republic of Kenya. So the 210 will remain but we have others.

We have added another main group of Parliamentarians to the members of the National Assembly. These members will be 90, I want to make it very clearly now in broad daylight, these 90 members are not nominated at all. Let me make this one very clear, these 90 members are not nominated at all, these members will be elected directly but what will happen is this, let me finish. As we were going all over the Kenya collecting views of Kenyans in all the 210 constituencies in this country, there were other groups of Kenyans which felt that their interests are not adequately reflected in Parliament. They said their views, their interests are not reflected. *WaBunge wakiingia huko ni mambo yao tu na kulala, sasa hawa walisema wao pia inatakikana mambo yao iwe wazi wazi na wao wenyewe wawe represented kwa Bunge*. So, who are these groups of people? These were:

- (1) Persons with disability – they felt that they need to be represented in Parliament.
- (2) *Vijana* – the youth, the youth felt that they also need to be represented in Parliament.
- (3) Marginalized areas – marginalized areas in our country also felt that its time, these include the ethnic minority. *Kuna makabila mengine kukiwa saa ile ya kupiga kura hawawezi kushida kwa sababu ni wachache*. So they also felt *wangukuwa represented kwa Bunge*. So these are the categories of people who were crying.

So for the sake of democracy, the new Constitution is saying why don't this Parliament be representative of every section in this republic of Kenya. Now how are they going to be elected? The condition is as follows: all the registered political parties in this country, be they 100 or 90 or whatever, all the registered political parties in this country shall submit a list of 90 people to the Electoral Commission of Kenya one year before they elections. Are we together? All the political parties in Kenya, be it Kanu, DP or whatever, they shall submit a list of 90 people to the Electoral Commission of Kenya one year before the elections. What will happen? There are very many tough condition to be fulfilled before that list is accepted. (1) That on the priority list we shall see on the top, we have the disabled, the youth, *akina mama*, marginalized areas, ethnic minority going down. It is only these people who will appear in that list of 90.

Now I'm going to the most difficult part where I'm requesting you to listen very carefully. How will this be done? (1) Every political party has submitted the list of 90 candidates to the Electoral Commission of Kenya. During the election day, wakati wa kura you people of Kenya will vote twice, are we together? Normally when you vote on a normal election day, somebody might say no, me I'm just interested in the candidate, so I'm voting for the candidate not the party, or somebody can say no, I'm just interested in voting for the party and not the candidate. But this time we want you to exercise full democracy, we want you to cast your votes twice, you will vote for a party and you will vote for a candidate. Are we together?

Now why are you voting twice? We want you to vote twice for several reasons. (1) You are voting for the candidate as the way you normally do but you are voting for the political party so that at the end of the elections the number of votes a political party gets, will determine the number of seats which are being allocated on those 90 people. Let me come again, for example, KANU as a party, KANU submit a list of 90 people, with disabled, the youth, marginalized areas and all others. Once KANU has done that, this is the election day, KANU will compete with other political parties, as they compete the total number of votes will be counted, isn't it? So the total number of votes KANU gets for example, if KANU gets 10% of the total votes in the whole country, we shall give it 10% of that 90. So 10% of that 90 is how many? Nine, so it means we are giving KANU 9 seats among the 90. But if KANU sweeps all the seats by getting a 100% of 90, we are giving KANU all the 90 seats but there are conditions which must be fulfilled. A political party is not just going to favour a particular ethnic group or a particular community, that list must have a national outlook, that list must have the disabled, the youth, the marginalized communities, in priority.

So that is the simple way. So it is not like it is a nominated member, yes, political parties will have to select, but during the voting day, you wananchi _____ (inaudible) of Kenya will have to vote directly, and whatever you vote for the political party, that percentage will be used against the total number of seats. Are we together now? I know you may not, some are still not understanding. I want to summarize Parliament as follows: The new Constitution is saying, Parliament will be composed of two houses, we shall have the National Council, baraza la kimataifa and it will compose of a 100 members, we have 68 districts plus 2 of Nairobi that is 70 districts, So we shall have 70 representatives in the National Council. The rest which are 30 we are reserving to women.

Then we have the National Assembly which is the current Parliament. In the National Assembly we are saying we shall have the 210 constituency Members of Parliament, but in addition to that we shall have 90 which is spread among the youth, the disabled, the ethnic minority, so that each group on the list is dominated by various groups of this country, and these shall be presented to the Electoral Commission one year before. During the election day, wananchi of Kenya will be called upon to vote twice, you vote for the candidate and you vote for the party. So the more votes the political party you are getting, the more number of seats you get out of the 90 seats. Are we together? So that is the position of this new Constitution. Some people have been saying that this is a very expensive exercise for Parliament. That may be true but in our position as a commission we

are saying, with proper management of resources in this country, this country is rich enough to maintain these number of people because at the end of the day each member in Parliament will represent all the views in this republic of Kenya. So that is in a nutshell what it is all about.

Having said that I want now to take you to devolution. Na ningependa tusome pamoja hii devolution inasema nini. If you have seen the page on devolution just _____it is page 26, devolution of power, that is chapter 10, page 26. Let us go to chapter 26 ili tusikie hii maneno ya devolution inasema nini. Devolution I would simply say it means bringing power or development closer to the people, that is in simple language. And I want also to say there are three points which the commission came up with. Having gone around all the constituencies in this republic of Kenya, wananchi felt that they are not participating fully in the services of the Government. Therefore they want to participate directly and actively in the Government.

So what the new Constitution says, there are three main objectives of devolution: (1) to bring development closer to the people of Kenya (2) to have equity in the distribution of resources (3) to have increased participation of Kenyan people in the management of their own affairs. Are we together? So let us read article 216 on page 26 which reads, levels of Government – powers are devolved to the following levels: (a) the village, (b) location (c) district and (d) province. What have we to say about village Government? Article 216 (1) The village decides whether the village council is constituted by village elders on two elections. (2) The village councils shall contain no less than 6 members and no more than 10 members. (3) The village decides on the system of village Government including the role of the village council. Are we together?

Then we have article 217 locational Government: It reads, the locational council consists of two representatives one of whom shall be a woman elected by each village council or among its members. (2) The locational administrator will be an Executive authority of the location. (3) The locational administrator shall be elected by the registered voters of the location. Are we together?

